



# Mradi wa OPTions

## Ombi la Mapendekezo ya mradi

Mradi wa Uvumbuzi wa Chaguzi za Utoaji Mimba (OPTions), Hatua ya 2

Novemba 2019

## **KUMBUKA: Maombi yatapokelewa kwa Kiingereza na Kifaransa TU**

### **TATIZO**

Zaidi ya utoaji wa mimba milioni 25 usio salama hufanyika duniani kila mwaka, ambapo asilimia 97 hutokea katika nchi zinazoendelea. Matokeo yake, takribani wanawake na wasichana milioni 7 wanapokewa kwenye vituo vya afya wakiwa na matatizo makubwa huku wanawake na wasichana 22,800 mpaka 31,000 wakifa kwa mwaka, jambo linalofanya utoaji wa mimba usio salama kuwa moja ya vyanzo vinavyoongoza vya vifo vya uzazi. Hata mahali ambapo utoaji wa mimba unaruhusiwa na kupatikana, ufikio wa huduma mara nyingi ni mdogo kutokana na vikwazo mbalimbali, na mara nyingi kuna chaguzi chache kuhusiana na njia za utoaji mimba. **Ufikio wa njia salama ya utoaji mimba ni jambo la msingi kwa usawa wa kijinsia na uwezeshwaji wa wanawake na wasichana.**

### **MRADI WA OPTIONS**

Lengo kuu la Mradi wa OPTions ni kuokoa na kuboresha maisha ya wanawake na wasichana kwa njia ya kuboresha ufikio wa njia salama na halali za utoaji wa mimba.

Lengo la **Ombi hili la Mapendekezo ya Mradi (RFP)** ni kuunga mkono **Mawazo ya Kijasiri yenye Matokeo Chanya®** kwa ajili ya ufikio wa njia salama za utoaji mimba kwa wanawake na wasichana wa nchi za kipato na chini na cha kati. Tunatafuta mbinu za kivumbuzi na kimageuzi zinazowaweka wanawake na wasichana katika nafasi ya kuamua ni wapi, lini na kwa namna gani wanatoa mimba zao. Hivyo basi, lengo la wito huu ni kuunga mkono uandaaji na ufanyaji majaribio wa: 1) **Mbinu mpya za kuongeza ufikio wa haraka kwa bidhaa na huduma zilizopo za utoaji wa mimba**, na 2) **njia za kisasa<sup>1</sup> za utoaji mimba**.

### **MAENEO YA KUZINGATIA**

Grand Challenges Canada inatafuta mawazo ya kijasiri yaliyobuniwa ili kutekelezwa katika nchi za kipato kidogo na cha kati na yanayolenga **ufikio wa njia salama za utoaji wa mimba**. Mawazo haya ya kijasiri yanaweza kubuniwa na mashirika yasiyo ya kupata faida na mashirika ya kupata faida, pamoja na taasisi nyingine zinazotambulika. Aina zifuatazo za taasisi ndizo hasa zinazohimizwa kutuma maombi na yataangaliwa kwa upendeleo katika mchakato wa mapitio.

- Taasisi zilizopo nje ya mtandao uliopo hivi sasa wa afya na haki ya masuala ya kingono na uzazi.
- Taasisi zinazoongeza thamani na kuleta mtizamo mpya katika nyanja ya utoaji mimba ulio salama.
- Taasisi zilizojikita katika kutambulisha njia mpya za kushughulikia tatizo lililotolewa katika Sehemu 1.2.
- Mashirika ya kijamii na mashirika ya kutetea haki za wanawake.

**Wapokeaji wa moja kwa moja wa zamani au wa sasa wa fedha za mfadhili mkubwa sana asiyefahamika hawana sifa ya kupata fedha za OPTions na wataondolewa kipindi cha mchakato wa mapitio ya wenye sifa.**

<sup>1</sup> Njia za kisasa ni njia zozote mbali na njia zilizopo na salama za utoaji mimba: utoaji mimba kwa kufyonza (MVA) na utoaji mimba kitabibu (MA).

Vumbuzi zinazopendekezwa zinapaswa kuwa **za kijasiri, za kibunifu, kimageuzi na ‘za tofauti’**, na zinapaswa kuwa na uwezekano wa kuboresha ufikio wa njia salama za utoaji mimba. Vumbuzi hizo zinategemewa kuboresha ufikio wa njia salama za utoaji mimba kupitia ama:

1. **Kuongeza ufikio wa haraka wa utoaji wa mimba kwa kufyonza (MVA)<sup>2</sup> na utoaji wa mimba kitabibu (MA)<sup>3</sup>.** Hii inajumuisha lakini haiishii katika mambo yafuatayo:
  - a. Kuongeza idadi ya watoa huduma wenye mafunzo na huduma salama zilizopo
  - b. Kuboresha ufikio wa taarifa zitakazomsaidia msichana au mwanamke kutoa ujauzito kwa njia salama
  - c. Kubadilisha mtazamo na kufanya suala la utoaji mimba kuwa kawaida ili kupambana na unyanyapaa
  - d. Kueneza na kutobagua utabibu wa huduma ya utoaji mimba
  - e. Kupunguza vikwazo vya kiuchumi vya kufikia njia salama za utoaji mimba
  - f. Kuainisha upya njia zilizopo za utoaji mimba ili ziendane na mifumo sahihi ya sheria.
  
2. **Kutambulisha njia mpya na salama ya utoaji mimba** itakayofanya maboresho muhimu ya aina moja au zaidi katika njia zilizopo, ikiwemo:
  - a. Uwezo wa kutumika kwa mafaniko katika hatua za baadae za ujauzito
  - b. Ufanisi katika utaoji wa mimba
  - c. Uwezo wa wanawake na wasichana kuifikia na kuitumia kwa uhuru na ufaragha mkubwa
  - d. Urahisi wa utumizi mzuri wa dawa (k.m. matumizi ya kidonge kimoja)
  - e. Kupunguza athari za dawa na maumivu
  - f. Uthabiti wa dawa
  - g. Ukubalikaji katika mifumo iliyopo ya udhibiti (k.m., ina viashiria vingine vya msingi)
  - h. Unafuu

Tafadhali zingatia kwamba huu ni muhtasari wa bidhaa lengwa kwa ajili ya njia za kisasa na salama ya utoaji mimba. Mapendekezo ya hatua za utabibu wa awali pamoja na hatua za utabibu yote ni halali, na malengo ya mradi kwa kipindi cha ruzuku cha miezi 18 mpaka 24 yataandaliwa ili yafae ipasavyo.

**Kumbuka: ni taasisi zilizosajiliwa kisheria katika nchi ya kipato cha chini na kati tu ndizo zenye sifa ya kutuma maombi katika eneo la kuzingatia la RFP la “kuongeza ufikio wa njia zilizopo za utoaji wa mimba”. Taasisi kutoka nchi nyingine zote, zikiwemo taasisi kutoka nchi za kipato cha juu, zina sifa ya kutuma maombi katika eneo la kuzingatia la RFP la “njia za kisasa za utoaji wa mimba.”**

<sup>2</sup> Utoaji Mimba kwa Kufyonza (MVA) ni njia ya upasuaji ya utoaji mimba inayoondoa tishu ya mimba katika mfuko wa uzazi.

<sup>3</sup> Utoaji wa mimba Kitatibu (MA) unatumia vidonge vya Mifepristone na Misoprostol ili kusababisha mimba kutoka.

## UFADHILI ULIOPO

Miradi itakayofanikiwa itapewa ruzuku ya mitaji hadi kufikia Dola za Canada \$250,000 kwa kipindi cha miezi 18 mpaka 24 ili kuandaa na kufanya majaribio ya uvumbuzi uliopendekezwa. Iwapo idadi ya kutosha ya mapendekezo yenye ubora itapokelewa, takribani misaada ya mitaji 20 itatolewa katika hatua hii.

## VICEZO VYA SIFA

Tafadhali pitia Vigezo vya Kufuzu katika Ombi kamili la Mapendekezo ya Miradi. Waombaji wenye sifa wanajumuisha mashirika ya kijamii na taasisi nyingine zinazotambulika ambazo:

- **si wapokeaji wa moja kwa moja wa zamani au wa sasa wa fedha za mfadhili wa kwanza wa Mradi wa OPTions.**
- zimeanzishwa na kusajiliwa kisheria, katika nchi yenye sifa, kama ibainishwavyo na eneo husika la kuzingatia la RFP ambalo taasisi inatuma maombi (tazama ukurasa uliopita)
- zinaweza kutekeleza kwa mafanikio shughuli husika kwenye eneo lao husika la kiufundi,
- zinaweza kupokea na kusimamia fedha za msaada.
- si wafanyabiashara binafsi.
- si ofisi mkazi za Umoja wa Mataifa.

Kila taasisi inaweza kutuma ombi moja (1) kwa kila eneo la kuzingatia la RFP (k.m pendekezo moja kwa vumbuzi zinazoongeza ufikio wa njia zilizopo za utoaji wa mimba na pendekezo lingine kwa njia za kisasa za utoaji wa mimba.) Kwa vyuo vikuu, pendekezo moja (1) kwa kila eneo la kuzingatia litapokolewa kutoka kila kituo cha utafiti kilichopo katika chuo kikuu husika.

## MAELEKEZO YA MAOMBI

**Maombi yatapokelewa kwa Kiingereza na Kifaransa TU**, na Ombi kamili la Mapendekezo ya Mradi linapatikana kwa **Kiingereza na Kifaransa tu**. Tafadhali pitia Ombi kamili la Mapendekezo ya Mradi kabla ya kutuma maombi ili kuhakikisha unakidhi vigezo vya kufuzu.

**MUDA WA MWISHO WA MAOMBI: Februari 11, 2020, saa 3:00 P.M. ET**

Kutokana na muda wa uchakataji, tunapandekeza kusajili akaunti kwenye Fluxx Portal si zaidi ya Februari 4, 2020.

Ili kuomba ufadhili wa fedha, waombaji WANAPASWA kutumia fomu ya maombi ya mtandaoni, inayopatikana kupitia Fluxx Portal ya Grand Challenges Canada ([gcc.fluxx.io](http://gcc.fluxx.io)) kwa Kiingereza na Kifaransa TU.